

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA SABA**

**KIKAO CHA AROBAINI NA NANE**

**15 JUNI, 2017**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA AROBAINI NA NANE – TAREHE 15 JUNI, 2017

I. DUA:

II. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

III. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

394. MHESHIMIWA SHAABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Wilaya ya Lushoto ni kongwe na ina Wananchi wapatao 550,000, kati ya hao kuna watu wenye ulemavu mbalimbali, Wajane na Wazee na wengi wao wapo Vijijini na hawajawahi kupata huduma za msingi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia makundi hayo ili nao waweze kupata huduma muhimu kama watu wengine.

**395. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Miaka ya 1980 kulikuwa na ushindani mkubwa uliojitokeza kati ya Shule binafsi na za Serikali ambapo Walimu bora wote walipatikana katika Shule za Serikali kutokana na maslahi bora ikiwemo posho zaidi nje ya mshahara kama vile posho ya ufundishaji, posho ya kupanga, posho ya usafiri na posho ya mazingira magumu:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya walimu kama ilivyokuwa miaka ya 1980 ili kuendana na dhana ya elimu bure lakini bora;
- (b) Je, Serikali ina mpango mkakati wa kuboresha zana za kufundishia ili kwenda sambamba na ukuzaji wa ujuzi wa stadi za taaluma wanazosoma;
- (c) Kwa kuwaombea walimu wapande mabasi bure kwenda kazini kama ombaomba kama ilivyotokea Dar es Salaam; Je, huku sio kuwadhalilisha.

**396. MHESHIMIWA MUSSA RASHID NTIMIZI  
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mabwawa ya maji katika Jimbo la Igalula hasa ikizingatiwa kuwa Jimbo hilo lina maeneo mazuri ya kutega Mabwawa ya maji.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**397. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN  
(CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kuongezeka kwa idadi ya watu na ukosefu wa ajira kwenye sekta zingine kumechangia sana Jamii kubwa ya watu kujikuta kwenye shughuli zinazosababisha uharibifu wa misitu kwa ajili ya kumudu maisha yao:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza udhibiti na ulinzi pamoja na upandaji miti nchini.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**398. MHESHIMIWA JOSEPHINE TABITHA  
CHAGULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Mkoa wa Geita hauna Chuo cha Ufundi (VETA):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Mkoa wa Geita.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA  
15 JUNI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**